



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA SIHA



Scanned with
CamScanner

Unapojibu tafadhali taja:
SDC/L 20/1/75
KAMISHNA WA ARDHI MSAIDI MKOA
MKOA WA KILIMANJARO
S. 1186
MOSHI

Tarehe: 12/12/2024

**YAH: OMBI LA KUFUTA NA KUPIMA UPYA SHAMBA UNIT 21
LENYE NAMBA YA UPIMAJI E⁵ 2176640-1188**

Kichwa habari hapo juu cha husika.

Tunaomba kibali cha kufuta ramani ya shamba tajwa hapo juu katika kumkumbu za serikali ili kuruhusu upimaji upya wa shamba hili. Shamba hili lilirejeshwa serikalini baada ya kununuliwa na Kampuni ya Kigeni inayoitwa COBBS na pia sehemu ya ekari 71 ya shamba hilo lilikuwa limevamiwa na wananchi kama mnunuzi wa shamba hili ameridhia kuachia sehemu iliyovamiwa kwa wananchi. Shamba hili sasa limeandaliwa mchoro wa mipango miji namba 04/siha DC/74/102023.

Pamoja na barua hii naambatisha nakala ya 'surrender' kwa ajili ya rejea yako.
Naomba kuwasilisha

JOSEPH MADANGI
KNY: MKURUGENZI MTENDAJI
SIHA
Kny. MKURUGENZI MTENDAJI
(SI) SIHA

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji, 5 BR-Sanya Juu-Elerai, S.L.P 129, 25482 Siha- Kilimanjao..
Simu: +225(0272)970677 Nukushi: +225(027)2970678
Barua pepe: ded@sihadc.go.tz Tovuti: www.sihadc.go.tz

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI

Simu: +255 27 2753361
Nukushi: +255 27 2753361
Tovuti: www.lands.go.tz



Kamishna wa Ardhi Msaidizi,
Mkoa wa Kilimanjaro,
S. L. P 1186,
MOSHI.

Unapojibu tafadhali taja:
Kumb. Na. SMD/KIL/SH/04/113

19, Desemba, 2024

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji Wilaya,
Halmashauri ya Wilaya ya Siha
S.L.P. 129,
Siha
Kilimanjaro

**YAH: MAOMBI YA KIBALI CHA KUFUTA NA KUPIMA UPYA SHAMBA UNIT 21
YENYE RAMANI YA UPIMAJI NAMBA E5/217/6640 LILILOPO SANYA JUU
HALMASHAURI YA WILAYA YA SIHA**

Tafadhali rejea barua yako yenye Kumb,Na.SDC/L.20/1/75 ya tarehe
12/12/2024 yenye kichwa tajwa hapo juu.

2. Ninapenda kukuarifu kuwa Mkurugenzi wa Upimaji na Ramani ametoa idhini ya kufuta na kupima upya shamba unit 21 lenye Ramani namba (Plan No) No. E5/217/6640 , , Yamekubaliwa kama ulivyoomba kwenye barua yako
- 3.Kwa barua hii unaelekezwa kupima kwa kufuata Mchoro wa Mipangomiji Na.04/SihDC/74/102023 uliyoidhinishwa tarehe 08/11/2023 na kwa kuzingatia Sheria ya Mipango Miji Na. 8/2007.
3. Aidha, Sheria ya Upimaji fungu la 16(1) Sura ya 324 zinatakiwa kuzingatiwa..


Esau S. Mwampashi

Kny: Kamishna wa Ardhi Msaidizi- Kilimanjaro

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI

Telegram: "ARDHI" –

Namba ya simu: 2753361

Nukushi: 027-2753361

Barua pepe: ael.kilimanjaro@lands.go.tz

Kumb. Na. LD/KLM/15790/11



Dfisi ya Kamishna wa Ardhi Msaidizi
26 Barabara ya Renguo
S.L.P.1186,
25101 MOSHI

15 Octoba, 2025

Mkurugenzi Mkuu,
Mamlaka ya Uwekezaji na Maeneo Maalumu ya Kiuchumi
Tanzania,
S. L. P. 938,
DAR ES SALAAM

**KUH: UFAFANUZI JUU YA MABADILIKO YA NAMBA ZA MASHAMBA NAMBA 336/9 NA
336/12 SANYA JUU WILAYA YA MOSHI KWENDA SHAMBA NAMBA 2203 SANYA JUU
WILAYA YA SIHA**

Sanjari na kichwa cha barua hii pia rejea barua yako yenye Kumb. CB.29/259/01/06 ya tarehe 08 Octoba, 2025. Ofisi ya Kamishna wa Ardhi Msaidizi Mkoa wa Kilimanjaro inakiri kupokea barua tajwa.

2. Kwa barua hii napenda kukufahamisha kuwa:

2.1 Wawekezaji wanaojulikana kwa jina kampuni ya COBBS EAST AFRICA LIMITED walinunua mashamba namba 336/9 & 336/12 kutoka Sanya Juu kwa ajili ya uwekezaji. Mashamba hayo kwa ujumla wake yalikuwa na ukubwa wa ekari 1071.

2.2. Baadaye ilibainika kuwa ndani ya shamba hilo kuna wananchi waliovamia kiasi cha shamba lenye ukubwa wa ekari 71. Hivyo Mwekezaji aliridhia ekari hizo ziondolewe aweze kubaki na eneo ambalo halitakuwa na mgogoro siku za baadaye.

2.3. Upimaji wa awali ulifutwa (shamba namba 336/9 na 336/17) (naambatisha barua ya maombi ya kufuta mashamba tajwa na kibali cha ufutaji kwa urahisi wa rejea)

2.4. Baada ya ufutaji kufanyika na kuondoa eneo lililovamiwa namba za shamba zilibadilika na kuwa shamba namba 2203 Sanya Juu wilaya ya siha lenye ukubwa wa hekta 385.65

Naomba kuwasilisha

Kny: Kamishna wa Ardhi Msaidizi
MKOA WA KILIMANJARO

NB: Wakati mashamba hayo yanapimwa kwa mara ya kwanza eneo hilo lilikuwa katika Wilaya ya Moshi, lakini eneo hilo baadaye liligawanyika na kuundwa kwa wilaya ya Siha ambayo ndipo mashamba yalipo kwa sasa